IBO IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

**SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SOUAHÉLI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SUAHELI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 17 May 2004 (morning)
Lundi 17 mai 2004 (matin)
Lunes 17 de mayo de 2004 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS


- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# CHUMBANI KWANGU



Mimi ni Jamila. Katika nyumba yetu, chumba cha sebule au baraza ni kikubwa kuliko vyote, na kila mara wazazi wangu wanakaa hapo na kuongea na wageni. Mimi ninapenda kukaa chumbani mwangu. Kila mara chumba changu kimejaa



rafiki zangu. Kwa jina la utani tunakiita chumba hiki ***kiota***, yaani nyumba ya ndege. Mimi na rafiki zangu ni kama ndege. Baada ya kutoka darasani tunaenda chumbani mwangu, tunakaa, tunazungumza, tunacheka, tunakula na kunywa, tunaangalia televisheni, na kadhalika. Baada ya rafiki zangu kuondoka ninabaki peke yangu. Chumba kinakuwa kimya kwa sababu kelele za ndege wenzangu hazipo tena. Wakati huu kiota kinakuwa kimya sana. Mara nyingi wakati huu ninaoga, ninasoma kidogo kitandani, baada ya kuchoka kusoma ninasali halafu ninalala na kuota kuhusu ndege wenzangu wenye kelele.

**KIFUNGU B**

## MTAA WA MADUKANI, DARAJANI, ZANZIBAR



Zanzibar,
Aprili 2004

Mpendwa Mama,

Pokea kadi hii nzuri ya Zanzibar. Picha hii ni ya Mtaa wa Darajani. Leo mimi na rafiki zangu tulitembelea mtaa huu maarufu wenye maduka ya bidhaa mbalimbali. Wenzangu wengi walinunua vitu vingi sana kama vile mabegi, nguo, tisheti, viatu, saa na hata redio. Mimi nilinunua vitu vichache kwa sababu bado sijapokea pesa ulizonitumia. Jioni tutakwenda kula chakula sehemu inayoitwa Forodhani. Sehemu hii iko kandokando ya bahari, na kuna vyakula vingi sana, hasa aina mbalimbali za samaki. Mimi, kama kawaida yangu, nitakula kuku na viazi vya kukaanga kwa sababu sipendi sana samaki. Lakini kabla ya kwenda Forodhani tutaogelea katika Bahari ya Hindi, halafu tutatembelea ***Jumba la Maajabu*** ambako kuna mambo mengi ya kuona. Vipi huko nyumbani? Msalimie sana baba na wadogo zangu. Ni mimi mtoto wako, Anita.


## KIFUNGU C: WATOTO WANAPENDA KUISHI MJINI AU VIJIJINI?



Mimi **naitwa** Renifrida Ngole (8), nasoma darasa la pili Shule ya Msingi Misewe.

Mimi napenda **kuishi** mjini sababu maisha ya mjini mazuri, kuna taa halafu nini vile kweli? Nyumba za mjini ni nzuri na za kijijini mbaya.

Mama akini**peleka** kijijini nitakaa kidogo sana.



Jina langu ni Steven John Minja (7). Ninasoma darasa la ngapi vile? Nime**sahau** dada, lakini St. Andrew.

Mimi napenda kukaa mjini kuzuri. Hapa mijini tunakula chipsi na nyama, kijijini nikienda sitakula chipsi na nyama. Mama akinipeleka kijijini sitakaa, kijijini hakuna taa.



Naitwa Catherine George (8). Nasoma shule ya *Hope and Joy* darasa la ngapi vile? Nimesahau. Mimi napenda kukaa mjini kwa sababu ni kuzuri. Kule tunasoma vizuri **tofauti** na kijijini kubaya. **Halafu** hakuna taa, kwa hiyo siwezi kuona usiku.


Nikiwa mkubwa nita**kataa** kukaa kijijini, nitakaa hapa hapa mjini na mama. Lakini watoto wa kijijini nawapenda.



Naitwa Emmanuel Alfred (12). Nasoma darasa la nne, Shule ya Msingi Misewe.

Mimi napenda kukaa mjini. Ni pazuri na kunachangamka. Kijijini hakuchangamki.

Mama akinipeleka kusoma kijijini nitakataa kwa sababu nimezoea kukaa mjini **kwani** kuna taa. Lakini watoto wa kijijini ni wazuri, wana**vaa** viatu kama sisi wa mjini.




Jina langu Frank Valentin (8). Ninasoma darasa la pili Shule ya Msingi Bunge. Mimi napenda kukaa mjini kwa sababu ni pazuri **pana** maghorofa, magari na nyumba nzuri.

Kijijini kubaya hakuna magari. Mimi siwezi kukaa kijijini nimezoea mjini, mama akinipeleka nitalia na kumsemea kwa **bibi.**

# KIFUNGU D: UNATAKA KUSAFIRI NA KUFURAHI?

Kwa nini usiende safari ya siku moja Bagamoyo
Kwa kutumia **HUDUMA ZA SAFARI ZA WANAFUNZI**?





| | |
|---|---|
| Tarehe: | Kila Jumamosi mwezi wa Juni. |
| Kuondoka: | Saa 2.00 asubuhi (kutoka Dar es Salaam) na kuwasili saa 4.00 asubuhi. |
| Bei: | |
| Nauli: | Shilingi 5,000.00 tu. |
| Malazi: | Shilingi 20,000.00 tu |
| Disko: | Shilingi 3,000.00 tu. |

Bagamoyo ni mji maarufu kandokando ya Bahari ya Hindi, Kaskazini- Mashariki ya Dar es Salaam. Huko kuna vitu mbalimbali kama vile nyumba za zamani na soko la watumwa. Pia kuna kanisa la zamani kuliko yote Tanzania. Hapa pia kuna Jumba la Makumbusho **lenye** vitu vingi vya **zamani.**





Ukiwa Bagamoyo unaweza kutembelea Chuo cha Sanaa. Kule utafundishwa kucheza ngoma, kuchora na kuimba. Soko la Bagamoyo lina vitu **mbalimbali** kama vile mboga, vyakula na aina nyingi za matunda. Kama unataka kuogelea basi karibu jiunge nasi twende wote Bagamoyo. Kule tutaweza kuogelea katika Bahari ya Hindi baada ya siku nzima ya kufurahi.

Jioni, baada ya chakula kutakuwa na Disko. Tutacheza kuanzia saa mbili usiku hadi saa sita usiku. Kutakuwa na mashindano ya kucheza. Unaweza kushinda na kupata zawadi kama vile *walkman*, simu ya mkononi, saa, redio ndogo, na kadhalika.

**KARIBU UJIUNGE NA KUFURAHI NASI. PIGA SIMU NAMBA +255 744 88 15 19**
**AU JAZA FOMU HIYO HAPO CHINI HALAFU ITUME KWA:**
**Huduma Za Safari za Wanafunzi, S.L.P. 35040, Dar es Salaam, Tanzania.**

✂..........................................................................................✂

Tafadhali nitumie habari na maelezo kuhusu safari za siku moja kwenda Bagamoyo.

Jina: ..........................................................................................
Anuani: ..........................................................................................
..........................................................................................
..........................................................................................